BAJUNI

# Shivulani ni Shaulani

**Mohamed M. Kombo**

TWAWEZA COMMUNICATIONS
Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association
Umoja ni Nguvu

SWAHILI RESOURCE CENTRE
Old Town, Sir Mbarak Hinawy Road,
Mombasa

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nd'a Twaweza Communications
Chapisho la Kwand'a 2024

ISBN: 978-9966-128-23-2

Kitabu hiki *Shivulani ni Shaulani* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha utamaduni wa Vabajuni. Nradi huu hutekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na Department for Digital, Culture, Media and Sport.

BRITISH COUNCIL

In partnership with
Department for Culture, Media & Sport

## Yaliyomo

Dibaji ........................................ 4

Shivulani ni Shaulani: *Kiunji cha Kwand'a* ........................................ 7

Shivulani ni Shaulani: *Kiunji cha Pili* ........................................ 14

Shivulani ni Shaulani: *Kiunji cha Chachu* ........................................ 22

Shivulani ni Shaulani: *Kiunji Cha Ine* ........................................ 33

Shivulani ni Shaulani: *Kiunji cha Tanu* ........................................ 39

Shivulani ni Shaulani: *Kiunji cha Sita* ........................................ 43

## Dibaji

Kitabu hiki cha ***Shivulani ni Shaulani*** kimechapishwa kutokana na mradi wa kulinda na kuimarisha turathi za Kibajuni unaoendeshwa na Shirika la Twaweza Communications pamoja na Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Mradi huu umefadhiliwa na Mfuko *wa British Council Cultural Protection Fund (CPF*) na ni hatua muhimu ya kutambua na kuipa hadhi lugha ya Kibajuni (Kitikuu) na utamaduni wake.

Nchini Kenya, Kibajuni kinazumgumzwa zaidi sehemu za Kiunga, Mwambore, Ishakani, Simambae, Rubu, Matironi, Mvundeni, Mkokoni, Shanga, Rasini, Faza, Tchundwa, Myabogi, Mbwajumwali, Kizingitini, Ndau, Mtangawanda, Ashuwei na Kiwaiyu. Pia kinazungumzwa nchini Somalia hasa Kisimaiyu na janibu yake. Wabajuni wameathiriwa na matukio mbalimbali ya kihistoria na kimazingira hasa vita vya Shifta vya 1964 – 1967 na vya miaka ya 1990 nchini Somalia na baada ya Rais Mohamed Siyad Barre (1919-1995) kung'olewa madarakani mnamo Januari 1991. Katika nyakati hizo za fujo na taharuki, Wabajuni wengi walifurushwa makwao na makazi yao yakabaki mahame. Hali hii imewaathiri hadi leo. Pamoja na hayo, kumekuwa na mabadiliko ya kijamii, mivutano, kupuuzwa kwa utamaduni na utovu wa maadili. Tungo nyingi za Mohamed Kombo (*Malenga wa SaYanga*) zimezungumzia maudhui haya huko zikirejelea turathi za Wabajuni na tungo za kimapokeo kama vile *vave* – ushairi wa jadi miongoni mwa wakulima.

Tungo za kimapokezi za Wabajuni ni pamoja na *vave***,** *randa, gungu,* na *kimai***.** *Vave* huimbwa wakati wa ukulima na kusaidiana kukata mwitu, kufyeka, kuchoma magugu, kupanda, na kuvuna. Ni utungo wa kushajiishana, kupana nguvu na moyo, ilimradi watu wafanye kazi kwa kushirikiana. *Randa* huimbwa kwa furaha na sherehe baada ya kazi ya kuchoma magugu kukamilika na watu kurejea nyumbani. *Kimai* ni utungo unaohusu mambo ya bahari na usafiri itokeapo ya kwamba mtu au watu wamepotea baharini. Ni njia ya kuwasiliana ana na yule aliyepotea baharini. *Gungu* asili yake ni malumbano na huimbwa katika sherehe za harusi. Tungo hizi za kimapokeo ni kisima cha sanaa na zimechangia pakubwa katika kuimarisha ushairi wa Wabajuni.

Mohamed Kombo hutunga hasa ili kuelimisha, kuhamasisha na kushajiisha jamii. Lakini si yeye peke yake afanyavyo hivyo. Kuna washairi wengine kama vile Athman Torah (*Malenga wa Lalavani*) na Abubaker Khuchi (*Ndhee wa Kibajuni*) wenye tungo za hali ya juu na wanaotumia jukwaa mbalimbali kuwasilisha ujumbe wao. Mumo humo katika kutetea lugha, tarihi na utamaduni wa Wabajuni kuna kikundi cha *Ndrimi Dha Kae* kinachofanya kazi pevu ya kulinda na kutetea turathi za kijamii. Uwanda huu mpana ndio unaompa Mohamed Kombo fursa ya kutunga na kuhamasisha umma.

Tangu mwaka wa 2020. Kombo ametunga kwa jina la *Malenga wa SaYanga* (Wimbi Kali). SaYanga ni kifupisho cha 'Sauti ya Ngaya'. 'Ngaya' bahari yenye mawimbi makali ipatikanayo baina ya visiwa vya Kiwaiyu, Ndau na Pate. Ni bahari isiyokuwa na utuvu, kama vile mashairi ya malenga huyu. Mashairi yake humfanya mtu kutafakari kuhusu yaliyomo na kuibua mazumgumzo katika jamii. Kama vile msafiri kutoka visiwa hivi hana budi kupitia wimbi la ngaya ili kuvuka ng'ambo ya pili, jamii ya Kibajuni inalazimika kuvumilia na kutafakari kwa kina hoja anazoziibua Malenga wa SaYanga ili ipate nafuu. Awali, Kombo alitunga kwa jina la *Malenga wa Ngaya Sounds* na *Jazzirian Mkombozi.*

Mashairi ya Mohamed Kombo yamechukua mfumo wa *uneni*; mtindo wa kimazumgumzo. Mfumo huu unampa uwanda mpana wa kuongea na hadhira yake moja kwa moja; kuisaili, kuiasa, kuihamasisha na kuizindua. Ni mfumo wa sanaa ya mkato inayoteka hisia za hadhira hasa pale mashairi yanapoghaniwa au kusomwa kwa sauti yenye mnato. Ushairi ni nyimbo zenye ujumbe unaowasilishwa kwa ufundi wa hali ya juu. Katika ufinyanzi wa ushairi, maneno huteuliwa na hupangwa ili yatoe mdundo wakati shairi linapoimbwa, linaposemwa, linapoghaniwa, au linaposomwa. Ushairi una uwezo wa kumfanya mtu ahisi furaha au uchungu; ridhaa au hasira; waweza kumburudisha mtu hadi moyo wake utulie au kumpa taharuki; ama kumhamasisha mtu aamue kuchukuwa hatua fulani ya kubadilisha hali, kama yafanyavyo mashairi mengi ya uhamasishaji na ukombozi.

Nilipomwuuliza Mohamed Kombo kwa nini anatunga kwa mtindo wa uneni alianiambia hivi:

> "…Sababu mojawapo ni kutaka hii fani ya ushairi ikuwe; sio tu kubaki pale ilipoachwa na waliyoigunduwa, bali na sisi washairi wa leo tuendelee kugunduwa mitindo mipya ya kuandika mashairi ili kuikuza zaidi hii fani. Sababu nyingine ni kutafuta njia bora za kuleta mawasiliano kati yetu sisi kama jamii. Ndio vile utaona mashairi haya ya UNENI huwa hayaimbwi kwa sauti ama mahadhi bali hunukuliwa kimazungumzo. Sababu ya tatu ni kutafuta njia ya kukuza mazungumzo juu ya mambo ambayo ni muhimu yazungumzwe na jamii katika ima kuyakuza mamboye, ama kuyarekebisha,na hata pia kuyapa nguvu mapya yaliyotujiya ambayo yana faida kwa jamii." (*Mazungumzo ya mtandaoni ya Oktoba 15*, 2023).

Shairi lake la kwanza kutunga lilitokana na uchungu aliouhisi baada ya kurudi nyumbani na kuona mtafaruku wa kijamii. Aliandika hivi:

*Iti kiilivacha, nalilivona kongo*
*Huu na ulee huchecha, na vangine ni misongo*
*Pungudhani machacha, musichuchapise nongo*

*Iti kiilivacha, nalilivona kongo*
*Vamoya huchecha, sababu dhiso mpango*
*Nyukani kumekucha, asokavoni ni tongo*

Kupitia ushairi wake, Mohamed Kombo amejitwika jukumu la kuinua jamii yake na kuipa hadhi. Anatunga mashairi na kuwasilisha ujumbe wenye maslahi kwa jamii. Anahimiza mazumgumzo ya kijamii kuhusu masuala mbalimbali na anatumia teknolojia ya habari kusambaza ujumbe wake. Ni mshairi wa kijamii anayerejelea tungo za kimapokeo kama inavyodhihirika katika shairi la *Shavulani ni Shaulani*. Tungo zake nyingine ni pamoja na *Vadhani Va Kiwaiyu* na *Mahavule na Jamii*. Tungo hizo zinapatikana katika mkusanyiko wa ***Mashairi a Kibajuni*** uliochapishwa na shirika la Twaweza Communications (2024).

Natumaini utafurahia tungo hizi!

***Kimani Njogu***
***Nairobi***

Januari, 2024.

## Shivulani ni Shaulani: Kiunji cha Kwand'a

1. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Mvumba dhivumbe
Kachupa fahamu

2. Kuyiva dhidhimbe
Na alipo maombe
Nadha nachi pembe
Dhisichudhulumu

3. Mvumba mocho urambe
Dha nn'edho na uvambe
Na mangi isi dhivumbe
Chuwafahamuo

4. Mvumba papa na simbe
Madondro na kh'ombe
Makoma na mahembe
Dhakula chuladho

5. Mvumba ith'i tungu
Mbinguni mavingu
Baharini mafungu
Kwauwedho wake

6. Mvumba dhiph'ingwa
Machochovu na nungwa
Namayumba kiengwa
Huvona shani lake

7. Navadhee vangu imi
Valo ufundra ulimi
Maneno avo tamami
Vachuwatiyeo

8. Namba sikomi
Kh'ele nadhivumi
Dhawavo ulimi
Valo changulia

9. Napia siatami
Th'adhivia ulimi
Vadhee vangu imi
Vakito nikubalia.

10. Bisumila nambe
Ruhu nidhipembe
Kwanyimbo niimbe
Shivu mukinishikia

11. Namangine nichendre
Uchu wechu niulindre
Tamad'uni dhivandre
Bid'ii chukidhichilia

12. Uchu wechu niupend'e
Tamad'uni nidhitund'e
Navainga nivadhind'e
Echu vasiakimbie

13. Ndrudha nivambie
Echu chusiakimbie
Chuwakumbachie
Akuchukudha

14. Malime chukalime
Ntonyi chukatome
Ilimu chukasome
Bila upingani

15. Mavuko valo hifadhi
Na malimo auyudhi
Vave kuchupa hadhi
Shukurani huvapachia

16. Hachuvatoi kh'ombo
Vaelewa vamambo
Valo imba nyimbo
Dhakuchuelea

17. Mema aurembo
Nidhidhuri dhombo
Kuchambia mwambo
Valo chuundria.

18. Bisumila nendre
Nlimani kh'apandre
Nidhienge kh'ondre
Dhalipo chulia

19. Kh'apandre nlimani
Nienge baharini
Dhilo maogeleshoni
Hadhiyatokea?

20. Nienge th'ini nlimani
Kulee valipo mararani
Vand'eevo miyani
Dhikoma vatanechea?

21. Kisha nienge pwani
Vana valee mbanyani?
Vaowavo ufuwoni
Kama vanaiya

22. Nienge na angani
Nocha mbinguni
Dhechu dhasafarini
Bad'o huchuvalia?

23. Nendre na makh'okoni
Kaenge dhombo ph'uluni
Akujengea kwechu miyini
Michi huchutind'ia?

24. Nishukie nyambani
Vatomao makingoni
Kh'amba dhimiyani
Namashambini hungia?

25. Ndrio muneledhe
Kisha munekedhe
N'nyani chunvudhe
Ruhusa kubakia?

26. Kinena sikidhani
Nan'i sinyamaeni
Huvaye ni n'geni
Kwavo alo asilia?

27. Midhimu ati
Vali nivanati
Chulivecheo iti
Valichuatia

28. Midhimu a angani
Nivalo mbinguni
Malaika a-Manani
Valo chuechea

29. Basi shikani shivu
Chukinena maekevu
Chuveni vachulivu
Echu kuwasikia

30. Chusikieni echu isi
Maneno en'e kasi
Anenwao na vapasi
Siechu asilia.

31. Bisumila chwendre
Ilimu chukavafundre
Dhembe vasipindre
Echu kuchufumia

32. Valee vasokayisi,
Vatafudhao uchesi
Navachiyao t'usi
Echu kuchuharibia

33. Makosa ni mikao
Asiasa dhivund'ao
Avave vapingao
Havayadhingatia

34. Avadhee vaachayavo
Nadhavo ila vaapavo
Nikuva dhuvo dhavo
Nd'akuhad'alia

35. Huand'ama upepo
Machao atokapo
Dhilemu dhilipo
Hudhikimbia

36. Upepo uvapekapo
Ndripo vendrapo
Boya dhingavepo
Hudhikimbia

37. Mavuko a Ad'amu
Isi chwaliafahamu
Ndrilo lechu ilimu
Hondreni hulimia

38. Mavuko aiti kh'uu
Kwavo Baba nkuu
Siya mwaka huu
Sikiani huvambia

39. Laliand'a lad'ini ilimu
Kwa a Musa kalamu
Kwake Muungamu
Likaya kutimia

40. Namba chusikidhaneni
Mashikio chaka chutoeni
Ndio ichuelee kwamakini
Vave ilo chwambia

41. Maneno tafusirini
Kwadhilingo siuneni
Mukaachia kufuruni
Ambao haavaelei

42. Van'ama chuvaengeni
Valisapo maholini
Kuvadhengea maholini
Nikupotea nd'ia

43. Makh'ulima hondreni
Matonyi echu baharini
Nao masomo chuvoni
Tafauti huchuelea

44. Nandra ahondreni
Ukond'o Wabaharini
Nakalamu achuvoni
Tafauti huivonea

45. Kisafiricho n'choni
Sikilo pwewa pwani
Kilioko maungoni
Hakiyatimia

46. Asoyiva mashalakh'oma
Na hondreni aso kulima
Utamad'uni kuto and'ama
Isi hachuto muwajabia

47. Aso kuchema mwichu
Asokula bisi nach'uchu
Wa ukh'ulima uchu
Atauwelewani?

48. Vave nikitabu
Nadhake irabu
Mwen'e kutulubu
Kuyiva huand'amia

49. Vave kwechu kh'wavo
Namuna chuipend'avo
Isi huiyand'ama ilivo
Maneno huchwelea

50. Vave ndrilo lechu ilimu
Amavuko kuwafahamu
Kwechu isi nimuhimu
Alee alochangulia.

51. Bisumila niye
Avave niasikiye
Akilini aningiye
Alivo muhimu

52. Neledhani muyivao
Mangi kuyiva nitakao
Nisokuva nafahamu nao
Kuayiva hubarikia

53. Madhuri alo tamu
Isi chukiafahamu
Amavuko na ilimu
Atachusaid'ia

54. Kwa luga ilo timu
Maneno tamamu
Naulimini nitamu
Chukiitamkia

55. Chuso ayiva chusineneni
Mageni mwechu ndrimini
Wala pia chusiapingeni
Kabula kuvulidhia

56. Kwand'a chuvulidheni
Chufasiriwe andrani
Ilimu hili la shaulani
Lipache kuchuelea

57. Nd'avadhee vechu
Valo ujenga uchu
Na mavuko echu
Kuchuhifadhia

58. Ilimu lakuchema
Kupisa nakulima
Vave kuiyand'ama
Hishima huvavekea

59. Kalendra a miongo
Niwavo ivo mpango
M'bajuni sitongo
Wakuvonywa nd'ia

60. Bisumila chwambe
Ilahi chumuombe
Achukinge nanyembe
Dhahii d'unia

61. Nyembe dhilioko
Hukh'acha mavuko
Na avadhee miko
Kuchuvund'ia

62. Nyembe tena mbovu
Huchupangia maovu
Kuchufanya vatwevu
Hudhikachalia

63. Echu chuwapend'avo
Ilahi chupe nasi ngavo
Audhalimu endre kwavo
Venye kuchutakia

64. Ilahi Rabi hukuomba
Ipachikanao mimba
Vadhawe vana simba
Khondre kuchulindria

65. Mana mwanasimba
Ndrie huva simba
Barani akachamba
Hadhi kuivekea

66. Ilahi ee Rabbuka
Navasidhawe n'oka
Dhidhadhi kuhasirika
Vakichuumia

67. Navadhawe verevu
Vapend'ao mavivu
Machundra maovu
Ven'e kuwatukia

68. Navaye vakombodhi
Vavashike makodhi
Kila kiuvi na kodhi
Kuchufukudhia

69. Navandroke vainga
Ven'e akili dhananga
Dhishikao ntanga
Kh'utu kumea

70. Chupe vachechedhi
Vadhisimamie aridhi
Ubajuni ake hadhi
Ipache kubakia

71. Chuechee ven'e nyoyo
Kivahudhunishe kiliyo
Pache kwechu makaliyo
Vaye kuwabikania

72. Chupe ven'e ghera
Vapend'ao aubora
Audhaifu kuvakera
Vasiaate kubakia

73. Rabi valee ven'e imani
Vachambuwavo hisani
Vaveke uwongodhini
Madhulumu kuadhivia.

74. Bisumila chwambiane
Ndrio chukumbusane
Alo echu chusiakane
Uwingani chukangia

75. Mila na tamad'uni
Dhechu Vabajuni
Chusidhimbirieni
Uwingani kungia

76. Arand'a na vave
Kwechu bora ave
Ndrisi isi ven'eve
Vakuihifadhia

77. Chusimameni vachuvone
Ndrudha chusikutamane
Aubajuni pache afane
Palee akichung'aria

78. Chuimbeni vasikie
Vave vaidhingatie
Ila ndrio vasiichie
Kwakuto kuvaelea

79. Chuneneni asikiwe
Echu achambuliwe
Na luga ihifadhiwe
Ipache kubakia

80. Echu chuaand'ikeni
Akisomwa dhitabuni
Uchambuliwe Ubajuni
Dharau kuukachalia

81. Luga echu asilia
Ndrimini ikibakia
Ni uchu kuitakia
Na kuichambuwa

82. Iso naluga sikabila
Hili halina n'jad'ala
Kibajuni hala hala
Hifadhi kukivekea

83. A nchu haivi ako
Utatekwa nnuko
Muengeni mbeko
Ake aishishievo

84. Ninchumwa asomila
Na uso maneno Tula
Ni n'domo wa dhela
Asikose kuchwelea

85. Bisumila na chuiyudhe
A Vadhee chusiapudhe
Na Ubajuni chuukudhe
Kama ulivo changulia

86. Kuva isi nivaongwana
Auchumwa huakana
Mila kwechu ilo fana
Ndrio huikumbachia

87. M'bajuni nimwelevu
Huuyidha upumbavu
Lakunfanya ntwevu
Wadhii hulikachalia

88. M'bajuni ni nchulivu
Hupend'elea wekevu
La kuichwa n'dhivu
Hishima humvund'ia

89. Wala Ubajuni sinusu
Siwanchu mahubusu
Ndrio mikono kuibusu
Vadhee chukivaamkia

90. Bisumila th'akoma
Kuipend'elea mema
Nikuivekea hishima
Kama valochangulia

91. Ni ahiri sumilani
Nipiche nlangoni
Ninenao Vabajuni
Chutaadhingatia?

92. Nendrao kwechu n'yini
Kwa vadhee majumbani
Avo valonao adhamani
Nami kh'aakumbachie

93. Mana imi ni M'bajuni
Nalo dhawa Bajunini
Ni Nd'odhi kisiwani
Ukovuche udhisiwapo

94. Nayiva nitokapo
Sitongo nendrapo
Usuli kulee ulipo
Ndripo kwechu

95 Ayivao chand'o nikipi
Ayiva ung'ongo siupapi
Chand'o hukipachapi
Aso kuva nacho?

*Hiyo hiyo hee!*

## Shivulani ni Shaulani: Kiunji cha Pili

1. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Duniani chuchambe
Mema kuitakia

2. Isi vote dhivumbe
Kwake chuombe
Isibakie chembe
Akudhulumia

3. Chuombe madhuri
Na nyoyo dhatahadhari
Mambo ene heri
Kuwabarikia

4. Chwambe bisumila
Kwa ina lake Mola
Akubikiwa salala
Asipache ndia

5. Madhuri chuachendre
Mema chuwapende
Kila lasifa chulitunde
Machafu asipache ndia

6. Chufanyeni mema
Chupache kwake wema
Maovu alochwandama
Apache kuchwandrokea

7. Kupendana chutakeni
Umoya chuubarikieni
Vabajuni chuichambueni
Mola tachusaidia

8. Namba haa nianene
Alioko chusiakane
Maovu asongemene
Mema huchukimbia

9. Maovu haalaniwi
Madhuri haatakiwi
Machafu haakimbiwi
Masafi huwatukia

10. Chubadilishidha nyendro
Dhichutewele dhishindro
Hadhichiliki tena pondro
Nkandra huchusikitisha

11. Hakutomeki tena Bori
Na kwainde echu bahari
Utonyi hauna udhuri
Mambo ndachubadilikia

12. Shauri lechu nigani?
Chuishivo dhisiwani
Matumaini utonyini
Mo huchupotea

13. Chutatedha nchaji gani
Kete hwisha dhichobweni
Dhakuchakachia sidhivoni
Shauri hulivulidhia

14. Maganga na akili
Valinena vataamali
Wamaudhiko uhamali
Hauyachuemea?

15. Bisumila chupime
Asuwapo kili dome
Ni ntonyi asintome
Yundu kinchilia

16. Kuvadha chusikome
Chukaivelea vame
Tadha vamwandame
Ashindwe kuvadhivia

17. Ntonyi na tome
Nkulima alime
Na mangine vaume
Kuwadhingatia

18. Dhichandrani chusivame
Vainde vaye vatume
Chutakuya kulia yomame
Kilo chechu kisisikiwe

19. Mbudhi vatalia meme
Na imbwa valulume
Haatayidha magome
Ayao kuwaketia

20. Mwene ulimi asiatame
Maonevu pache asikome
Talia nchume mame
Huruma asifanyiwe

21. Akimbidhiyeo nasimame
Mbio dhake dhikome
Asichukie ng'ombe tume
Maafa kuitakia

22. Bisumila chudai
Hachukufa chuko hai
Haki dhisandame mai
Chukishuhudia

23. Avao khondreni mwechu
Chupache fungu lechu
Asichudhulumu nchu
Kwechu aloguria

24. Dhivunwadho kh'ondreni
Apache haki ake M'bajuni
Vasiatiwe vageni
Haki kudhivamia

25. Kulipwa ive sharia
Aridhi echu kuichumia
Hili chusipo libikania
Venyeji chutayuti

26. Haki hadhikuisita
Kudhidai chukiata
Dhitakuva t'ata
Udhio kutomewa

27. Chusiveni malenge
Chukava burukenge
Maboma asengenge
Akachuhasiri

28. Chusiveni mipiso
Chukakosa maso
Chukaveshwa leso
Chukiangalia

29. Kwambiana kuko
Kusikidhana kuveko
Pandi havi boko
Angapendelea

30. Nasi kwechu chulipo
Hachupichi siupepo
Hudaiye phopo
Kuchutawalia?

31. Bisumila chueledhe
Mwene suwali avudhe
Usawa vasiupudhe
Vene kuusikia

32. Chuvaeledhe ausawa
Vapache kuwaelewa
Ruhu kuchuchafuwa
Chuvakachalie

33. Kila nchu na kwavo
Ndrivo dunia ilivo
Kunipoka kwangu sivo
Nimakosa huvambia

34. Kwechu chuiyelewe
Ndechu mahaliwe
Chuyive chusihadawe
Chukapotedhwa ndia

35. Chuveni verevu
Chuwate ukulivu
Mambo kwa wekevu
Chuwasimamie

36. Mwanati na n'geni
Kihaki havafanani
Kote ulimwenguni
Hili huchambuliwa

37. Wa n'geni urongo
Usichufanye mirengo
Hachuyava tongo
Vakuvonywa ndia

38. Hakivi changu chako
Changu imi sichako
Kuchasuwa hili sinchafuko
Wala sikutukia

39. Kutaka haki siutukivu
Kutoitaka ni upumbavu
Nachusipokwe uchulivu
Chukinena chukatukiwa

40. Uwanati chuufahamu
Nihaki akibinadamu
Kuchambuliwa iladhimu
Kwene katiba na sharia

41. Aridhi dha venyeji
Niushetwani kudhihoji
Mungu ndrie mpaji
alo chuavanyia

42. Avanati makao
Kila kabila inao
Avangine anyakuwao
Uwadui hubarikia

43. Bisumila chutake
Kwechu kuchambulike
Sharia iladhimike
Kuchuhifadhia

44. Chuneneni chusikiwe
Chutakao chufanyiwe
Sharia chuvekewe
Kwechu kuchulindria

45. Uwonevu chuyidheni
Vayavo vasichuhini
Vakaribie kwa amani
Uwanati ubakie

46. Chusiechewe ubagudhi
Likakosa kuchuudhi
Chutakuva vapudhi
Chudhulumike

47. Ukabila chuudhivie
Amu chusiuvumilie
Kulee utokapo urudie
Usichuharibie dunia

48. Huecha mangi akuudhi
Dharau huipa ngadhi
Dhuluma kava uwamudhi
Ikachafuka dunia

49. Ukabila ni ubagudhi
Dharau ni uchokodhi
Dhuluma ni uvamidhi
Uchafu wa kidunia

50. Ukabila ni uritadi
Kunena kweli hubidi
Ukiatwa nchini kudhidi
Amani tachuharibia

51. Na udhiviwe ukome
Kuchambuliwe kwa mame
Si kwansuwa kili dome
Amani asichuharibie

52. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Alokachadha udhembe
Kwene dunia

53: Chwambe bisumila
Udhembe ni ila
Usifanywe mila
Ina kuchuharibia

54. Namba asikike
Anenwao afahamike
Sahauni chusiadhike
Kuto adhingatia

55. Udhembe ni ugonjwa
Mwenenao hutengwa
Ukintawala hutungwa
Ng'ombe wamaridhia

56. Namba n'dhembe
Hulidhanya yembe
Kanunuwa wembe
Nee kunyolea

57. Huidhulumu Yumbe
Akabikiwa pembe
Bwanaimi asambe
Huku nkudhia

58. Jamani udhembe
Huchofa ni chembe
Chusiupe kipembe
Numba tachuvundia

59. Chuhadhari na udhembe
Usichufanye ng'ombe
Chukamea pembe
Kuichukia dunia

60. Namba udhembe
Kama uteeoni tembe
Chuutunge usichambe
Mila kuchuharibia

61. Bisumila chuvadhe
Masuwali chuvudhe
Chusokaayisi chusipudhe
Chukabaki uwingani

62. Chusianyamisie dhikosi
Mapia chusiyo kaayisi
Tachudhuru mpasi
Upenyu kumwatia

63. Chutakeni kuyiva
Isichuchofe miva
Chukalia huvava
Utungu chukiusikia

64. Kuyiva ni werevu
Hukimbidha utwevu
Kadhivia uwovu
Usipache ndia

65. Chuvadheni kwa makini
Huu wechu isi Ubajuni
Chutamwatia nyani
Kuchuangalilia?.

66. Kinya chusikishabiki
Uwingani chukabaki
Kisha dhechu haki
Dhikatukuliwa

67. Mavadho ni muhimu
Tena niikuru ilimu
Mambo kuwafahamu
Huladhimu kufikiria

68. Chusive mai kuwandama
Pwani kuyaa na kufuma
Mwana huva nchu ndhima
Ujana ukimuishia

69. Kila alodhawa hufa
Dhikatukuliwa nyadhifa
Isipokuva sifa na kashifa
Hakuna wakunrithia

70. Chukivadha mema
Atachuchia huruma
Dhichuepuke suhuma
Amani ikibakia

71. Chukivadha maovu
Tachufanya vatukivu
Uchutawale utwevu
Uwinga kubarikia

72. Na usipotee bure muda
Chuvadheni ene faida
Ahapa duniani na ibada
Ene kuchusaidia

73. Bisumila chuichambuwe
Kwa echu ndrio chuikuwe
Ubajuni usidharauliwe
Chukainyamalia

74. Chuutukudhe utukuke
Kwa nyendro dhiso mivuke
Irudi tena hadhi ake
Kama ulivo changulia

75. Chuveni vakweli
Urongo chusiukubali
Chukavekewa badali
Akili kudhunguliwa

76. Chuukudhe uwongwana
Wavadhee uloyivikana
Ndrio chutachambulikana
Echu chukiasimamia

77. Chuitukudheni mila
Dini chusiichieni ila
Anyuke kila alo iyala
Ubajuni kuuwangalia

78. Chukito ichambuwa
Hachuto chambuliwa
Usokaelewi elewa
Imi kweli hukwambia

79. Chukito itukudha
Kwa akupedhedha
Ayao atachupudha
Chubaki kuililia

80. Ikudhe ndruwa ukuwe
Ndripo uchambuliwe
Ndiani usandrolewe
Kama uchafu wandia

81. Bisumila sikidhani
Nnene chusokaambiani
Achuveseeo kidhani
Muwanga kuchukimbia

82. Mambo chuchendrao
Maishani achudhuruo
Kwa ajili amikao
Isi huwabarikia

83. Mambo tena maovu
Achufanyao vatwevu
Huvae vapumbavu
Chukaap'apalia?

84. Mambo akihuni
Achuchiyao aibuni
Kwa ajili aushindrani
Huwapelea ndia

85. Kama mikao siasani
Makundri mwechu miyini
Madhihabi kwene dini
Miyi huchuvundia

86. Ubinafusi uwongodhini
Umoya hautakikani
Vamoya havapendani
Udhaifu huubarikia

87. Ushirikina huusamini
Chukaidharau echu dini
Akurogana na majini
Wendrapo taasikia

88. Ubaringanya na widhi
Hubarikiwa halichuudhi
Vafanyao nivayudhi
Mabaradhani husifiwa

89. Dhama dha kuvunda
Ndridho hudhipenda
Chubarikiyao uyinda
Miyi huchuvodhea

90. Bisumila chupime
Alochwechea Nchume
Nahaa echu milume
Ni api akuchusaidia?

91. Dhiki chulidhonadho
Ni kubarikia mivodho
Dha dini dhake ngudho
Mutwa huchulia

92. Chumbiridhie tamaduni
Mila eo hachuisamini
Udhuri kwechu ni uhuni
Ukiya huukumbachia

93. Ndrio kuwenea taharuki
Chukava hachuchambuliki
Hudhiviwa dhechu haki
Na hachutaki kudhingatia

94. Ukilima wimbi
Huvuni tambi
Na achao idhimbi
Bahari taitungia

95. Iyema mwichuni
Lingachegewa noni
Halinshiki mbuni
Sababu huchwelea

96. Kuto kuyiva kufanya
Hukosa dhakuwavanya
Ndripo nchu wamwanya
Kianga akadirikia

97. Akifanya kutoyiva
Mbavaa kantaba teva
Tadhandra kamuova
Mauti huitakia

98. Haa mambo simadhicho
Kuwaelewa haana uchocho
Avonekanapo mapicho
Hupichwa kava ndia

99. Chuveni na taamali
Na madhingatio kamili
Chusidhunguliwe akili
Aubora kuwakimbia

*Hiyo hiyo hee!*

## Shivulani ni Shaulani: Kiunji cha Chachu

1. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Mvumba dhivumbe
Kunsujudia

2. Mungu kumuomba
Hata tangumamba
Na barani simba
Hutegemea

3. Bila amuri ake
Hauki nk'eke
Uwedho mbwake
Ilahi Mola Jalia

4. Kuomba chusichoke
Matumaini k'wake
Wala chusighurike
Chukapotea ndia

5. Kumuomba Mola
Ive kwechu aula
Usiku chukiiyala
Nachukinyuka pia

6. Bisumila chupende
Ibada chulichende
Amuri chusivunde
Mema chukitarajia

7. Chusikieni amuri ake
Chufanyeni ibada lake
Chukitegemea kwake
Haichuhadai dunia

8. Mana ndrie mfalume
Hakuna kwake dume
Vafidhuli navakome
Maangamivu kuitakia

9. Hakuna bora bwana
Kunshindra Maulana
Hili mwene kulikana
Niibilisi navambia

10. Uchuvumbie dhivumbe
Ulimwenguni chuchambe
Ela n'ngine chusimuombe
Na akufuru kuwabarikia

11. A Mungu chuwakubali
Na anchume chuwajali
Avadhee ave niwahali
Kuchuongodha ndia

12. Vadhee chuvahishimuni
Mema chuvachendreeni
Valosumbuka maishani
Kuchudhaa nakuchuwea

13. Umuri chuuchambueni
Udhee chuusaminini
Ujana usichuhadaeni
Udheeni utasilia

14. Usivone undakuwa
Ukasahau ulidhawa
Udhaoni ulitukuliwa
Mimba nyedhi tisia

15. Kivekoni katukuliwa
Chakula katafudhiwa
Nguvo ukanunuliwa
Sisahau nakwambia.

16. Bisumila chudhingatie
Kupudha chusibarikie
Avao nachuwaangalie
Kwa ito lakufikiria

17. Chwengeni mambo alivo
Kwechu miyini apekwavo
Ndrivo isi chuwatakavo
Mbona huwanyamalia?

18. Chudhingatieni chuyive
Maviti huvaye asivive
N'gonjwa dawa asituve
Sababu chundaifikiria?

19. Chusiachuswe chukacha
Wala chusitakeni dhicha
Ela la nanga kukokocha
Chusikubalini navambia

20. Chombo kitafuwawa
Usafiri utambiriwa
Akosapo kudhingatiwa
Mambo huharibika

21. Chikiregea kumbuka
Kifundro hufunguka
M'bajuni aliatamuka
Haa kuchuweledhea

22. Hupachilidhwa uvuongo
Ulimai,nalifikirie bongo
Ukikauka ni urongo
Kijungu hutafanyia

23. Mwene mato sitongo
Anganyamisa shingo
Ichendrekao mipango
Mato huiyangalia

24. Hupiswa ikikauka
T'ange ilochemeka
Rigombo ikavaka
Mosi ukaenea

25. Kitanga naivu
Humpa uchulivu
Kapumuwa utovu
Nkulima kaisonea

26. Mbeu kadhitauwa
Akiiyongoja vuwa
Hondreni kuyawa
Mavuno hutarajia.

27. Bisumila mbee ndoni
Mangi chueledhanyeni
Umoya huukachaliani
Vadhee valo chuusia?

28. Umoya ni nguvu
Utengano ni utwevu
Huvaye vapumbavu
Ubora kuukimbia?

29. Umoya ni wekevu
Ndrio kuva verevu
Hufanyiwae utukivu
Vene kuupendelea?

30. Umoya ni muhimu
Hutimidha majukumu
Mbona huidhulumu
Kuto kuukubalia?

31. Na chudhungumudheni
Achudhikio chuwayiveni
Udhaifu chuuweleweni
Uchudhiviliyao ndia

35. Chusichoke chwambe
Pache unyowe wembe
Goma ndio lichambe
Utamaduni kuubarikia

36. Chusitafudhe dhipembe
Dhakuisita dhivumbe
Kama ipwani k'ombe
N'tanga kuifutia

37. Chuundreni tena dhombo
Chuutembeeni mwambo
Ubajuni wake urembo
Chupache kuurudishia

38. Chwali nivachu huru
Kwa majahadhi makuru
Chukisafiri bila aruru
Hakuveko wakuchudhivia

39. Alikuvae nsafiri
Alotawala bahari
Kudhiviwa akakiri
Usafiri kaumbiria?

40. Kinena dhombo chuundreni
Niuwongodhi wechu Vabajuni
Ubajuni ndrio chuusimamieni
Urudi ulivokuva dhamani

41. Haa ndakudhingatiwa
Mambowe akajadiliwa
Echu kuto kukubaliwa
Chushishie nchi gani?

42. Akikosekana mauwa
Kugura huladhimiwa
N'oki wakutarajiwa
Makulima kuwasaidia

43. Naomba shivu shikani
Yapo uvuvudhi wandrani
Kimwa hela sinyamaeni
Pweke mukanatia?

44. Chuutukudheni Ubajuni
Nadhake tamu tamaduni
Bidii chuhimidhaneni
Ake kuwabarikia.

45. Bisumila chusisahauni
Alopicha chukumbukeni
Achusaidie nasi safarini
Fahamu kuchuchia

46. Nakila siku avao
Mambo achendrekao
Alee chuwapendao
Nachusokaapendi pia

47. Palee chukiakumbuka
Nakuvadha chukataka
Basi akili dhitafunguka
Fahamu kuchungia

48. Laligaukaye umbo
Irara kava kichembo
Kuchwelea hili yambo
Mavadho husaidia

49. Chukikielewa chando
Chauvumbudhi wa t'indo
Chutaayiva ake matindo
Chutakiwao kutindia

50. Chwaiyiva sababu
Alengo matulubu
Numba kuva wajibu
Ni sitara huitakia

51. Palee chukifahamu
Chukayiva umuhimu
Chutaata kuidhulumu
Ukombodhi kupendelea

52. Chukitaka kubadilika
Kwanda nkurakibika
Haki dhikichambulika
Maisha tachung'aria.

53. Bisumila chwendreni
Kwechu kulee miyini
Kwa vadhee milangoni
Chuikuwe chukisikilia

54. Chuupingeni upweke
Pache udharaulike
Ushirika chuutake
Umoya kuubarikia

55. Ubinafusi utengeke
Kama uyusi unuke
Miyini uwondroke
Ukose pakukaribia

56. Mana uchutawalie
Bajunini kuharibisie
N'nyani isi chuntapie
Ubinafusi kuudhivia?

57. Ndrisi vakuudhivia
Miyini usipache ndia
Mwene nao akitapia
Asiwedhe kuuchumia

58. Chutaudhiviyae huvudha
Ubinafusi undao kuvodha
Mashauri akipendedha
Huva tamu akichumiwa

59. Chusikidhane chukieledhana
Chuwachumieni ene maana
Faida palee ikipachikana
Ubinafusi utakimbia

60. Ulipachae ndia
Ubinafusi kuvamia
Umoya ukakimbia
Ushindrwe kuudhivia?

61. Siingine nvambie
Kudhia ichuhadadhie
Huvona chusuluhie
Udhivu kuubarikia

62. Ndanini kufanya kadhi
Mwanadamu kuiyudhi
Alee adhiuvi na kodhi
Ni rahisi kupachia

63. Huu ndrio mwendro
Undao mea k'ondro
Unvonao dhishindro
Hukimbilia kudhia

64. Huku ndrio kwerevuka
Usindidhini kutoka
Jamii kudhulumika
Ubinafusi kwendrelea

65. Dhajamii vadhitaka ivo
Ndrivo vadhivu valivo
Yapo na nguvu dhavo
Kadhi hudhikimbia

66. Vaendeme makochi
Vako tini amabuchi
Kulivachwa havachi
Kudhia hubarikia.

67. Bisumila chusipudheni
Auvumi na aushetwani
Adhungukao miyini
Amani kuchuchafulia

68. Ni aeneeo Bajunini
Aushiriki wa majini
Kimwa chusinyamaeni
Ni kuwabarikia

69. Kama ako naadhiviwe
Na hatuwa atukuliwe
Uvanda na asiatiwe
Kuichafuwa dunia

70. Kama hakuna niuvumi
Huvaye lisivekwe ikemi
Dhikava hutinda ndrimi
Hachuchoki kudhisikia?

71. Sipingi kuva ako
Siungi ave ataveko
Lambiwalo liko liko
Vadhee valichwambia

72. Lakini lililoko nigani?
Pache chulifahamuni
Ndrio chulidhivieni
Kuchafuwa dunia

73. Nakama ote mavili
Ako,chusiakubali
Chudhivieni ujahili
Usichuharibie dunia

74. Nakama ote niurongo
Huwatiwaye ulingo
Asikachiwe dhilingo
Kero kuchwandrokea?

75. Ushiriki kwelii niharamu
Hukachadhwa vaisilamu
Lakini isi chwafahamu
Vako vakuubarikia

76. Naurongo nidhambi
Hakuna vasokaambi?
Chukinena hachuambi
Nilipi basi hulibarikia?

77. Kama widhi niharamu
Chudhividhiwa vanadamu
Vajep'ao chukivafahamu
Widhi chutavakania?

78. Na ushiriki nikufuru
Umedhiviliwa uhuru
Ukifanywa hudhuru
Sihaki kuunyamalia

79. Chwauyiva nikufuru
Tena dhambi dhikuru
Na upokwe udhuru
Maovu kuchuvamia

80. Kuva uko uko
Navashiriki vako
Vakuudhivia vaveko
Uvanda kuufungia

81. Ni varitadi vaufanyao
Ni maaduwi vaukubalio
Nauvapee sasa upeo
Uchafu wakidunia

82. Naiveko hatuwa kali
Kuudhivia huu ujahili
Kunyamaa nikukubali
Amani kuchuchafulia

83. Haa mambo alivo
Nihatari aatwavo
Naachiliwe kiovo
Nshipi kuvavuchia

84. Nadhichegewe jarifa
Dhishikwe kashifa
Achuondrokee maafa
Kufuru na kudhia

85. Naashikwe kwa iyema
Asifanyiwe huruma
Chukiitaka salama
A Mungu nikuwasikia

86. Chuwavekeeni nchambo,
Mena, dhembe na ulimbo
Atapiliyapo kwene imbo
Asilaumu akiumia

87. Riba ni dhambi
Lakini huliwa tambi
Huchandrikiwa jambi
Dhikafurahiwa

88. Lamajini nihiya hiya
Dini yapo hulidhiviya
Sikuva halina ndiya
Varitadi hulichumia

89. Chusilikubalini
Chusilipudheni
Chulichambueni
Chulichachueni

90. Kwendra kinime na Mola
Andachusikilia madhila
Hachunyuki chulo iyala
Avao chukaangalia?

91. Hawishi ukele wamai
Chufie chungali hai
Madhuri huwatumai
Haramu kuwasikilia

92. Maisha eo haaishiki
Dhichu hadhinunuliki
Nakukubali hachutaki
Kwa Mola chukarudia

93. Dhichuenee sasa dhiki
Hadhishi ningi taharuki
Chuwatakao haachutaki
Haa huwadhingatia?

94. Ndakuva tenge tahanani
Wala hachuchambuwani
Unvonao ni mato upaani
Munkari wataka kuukia.

95. Bisumila chwambe
Duwa chudhiombe
Uhasidi usichambe
Chukaunyamalia

96. Mana uhasidi nimuovu
Tena nitabia ilotwevu
Kuhusudu ni utukivu
Ndruo kumfanyia

97. Kuwatukia andrudhako
Kuva haakuva ndako
Likuchie nno maudhiko
Ni uhasidi nakwambia

98. Kuchayana kwa uwovu
Kutawaliwa ruhu nawivu
Kupendeleana maovu
Ni uhasidi huvambia

99. Uhasidi ni kiito
cha mpereketo
Hujenga dhitoto
Dhakuchafulia

100. Kuto kupendeleana
Madhuri ene kufana
Maovu chukatakiana
Ni uhasidi huvambia

101. Imi sina nae asipache
T’anchilia ntanga nkache
Nin’dhivilie nandia asipiche
Huu ni uhasidi huvambia

102. Nalisive kila lifanywalo
Asichengekewe umbulo
Nibora utune ngololo
Ni uhasidi hukwambia

103. Ulee jamani huvae
Alonao kupacha nae
Ndrio eo mavadhoe
Kwechu alobakia

104. Haa ndrio aliyoko
Ajengao maudhiko
Nakuchiana mboko
Dhauhasidi vendani

105. Hiya basi kutaishika
Uhasidi ukikubalika
Kwechu hakutakalika
Vangi vatakimbia

106. Chutakimbilia kwapi
Ikiva ukuchi na upapi
Hakuna labora ni upi
Dhitaepukanae?

107. Haa isi chukianena
Sikutaka kuudhiana
Alioko hukumbusana
Miyi huchuvundia

108. Kufuru huchwangamidha
Hudhuru miyi huivodha
Sikasirike akikuemedha
Gaudha ulonao tabia

109. Kama hufanya ata
Udhio siuvundie t'ata
Na vaeyavo mabita
Sitake kuvaharibia

110. Kuikuwa nao niudhalimu
Kuva undakuvelea tamu
Yiva kwa Mungu hukumu
Wendrapo hutaikimbia

111. Amajini na adhiviwe
Asiendelee mambowe
Miyini ruhu dhichuwe
Akichuwandrokea

112. Kama hufanyi sinyamae
Vakuchayavo sivakubalie
Vakanye wasiwasi usie
Nasi amani ichuyie

113. Kimwa huchia shaka
Uchaywapo ukaridhka
Usijali kuva huchayika
Ni api atafikiriwa?

114. Auhasidi na anolewe
Uvanda na asiatiwe
Afanyao biri aukiwe
Miyi asichuchafulie

115. Vafanyao ote navakome
Vanswaliye wavo nchume
Shetwani vasimwandame
Mochoni kuvatugidhia

116. Kama alikuva ni simba
Angalijengewa kirimba
Hangaliatwa kuchamba
Pundra kuchumalidhia

117. Kama alikuva ni p'isi
Angalinolewa nlanisi
Hangaliatwa mwasi
Mbudhi kuchulia

118. Kama angalikuva niuk'eche
Angalivindwa n'yini asipiche
Ama avuwawe nk'ukuche
Akose k'uku kuchulia

119. Huvaye huu udhalimu
Uchudhikiyo vanadamu
Chukaata kuuhukumu
Uvavo chukauwenga?

120. Vanenao ako kuvaamini
Na vaapeke sirikalini
Udhiviwe ushetwani
Miyi kuchuvundia

121. Atani nvakumbuse
Asokataki apukuse
Lakini asimuachuse
Mambo kim'badilikia

122. N'dhingadhinga hukucha
Apambanapo na dhicha
Husumuka ake mak'ucha
Kudhingadhinga akayutia

123. Na mwenendi hukuvaa
Dhikatoka dhake dhijaa
Dhiachu akijaribu kuvaa
Utungu akausikia.

124. Bisumila nambe
Vabajuni nivaombe
Ubajuni chuupambe
Sifa dhakupendedha

125. Ndrio imi kaanda
Mavindoni kuvinda
Vanama kavatinda
Kama valo changulia

126. Ubajuni kuusifu
Nichuve nadhwifu
Kila la upochofu
Isi kuukachalia

127. Ubajuni uchu wangu
Pia mbwako nduangu
Alochupa ni Mungu
Afaa kudhingatia

128. Ubajuni ni damu
A Hawaa na Adamu
Haikachi mwanadamu
Isi kuchutavanyia

129. Ubajuni niuwongwana
Sifa dhakuyivikana
Wakuuchafuwa hakuna
Chukiuchambuwa

130. Ubajuni huunyuwa
Sikomi kuukunduwa
Siati kuuchambuwa
Alinipa Mola Jalia

131. Ubajuni chuyive ndriwe,
Nami chuuchambuwe
Pache usidharauliwe
Likakosa kuchuudhi

132. Ubajuni chuufahamu
Kwamema chuuhishimu
Chuyidhe akuudhulumu
Kwechu kuchuyia

133. Chuupende kwadhichendro
Chuukachalie auvundro
Chusiveni kononi chondro
Dhidak'o chukaubikia

134. Shirindovu ukintapia
Ukanlivacha, nayeda pia
Hukuchofa ukakamia
Huyidha kuvonewa

135. Huchufundra madhingira
Mifano kwechu ilobora
Kuichechea haivi niukora
Usalama wako kuitakia

136. Sharia amaumbile
Ninoni amee mbale
Simba magugu asile
Ndrivo ilivo dunia

137. Kila nchu unapake
Kwechu kuchambulike
Kuchupoka asitake
Kwavo aloshikilia

138. Haki dhechu chutake
Bajunini dhisidhulumike
Vene nguvu isikubalike
Dhive ndavo kudhivamia

139. Alotajiri na alomasikini
Vave sawa maamudhini
Kama vendavo kaburini
Na udhaoni valivotoka

140. Hii ndrio midhani
Ake Mola Rahamani
Kuikubali Vabajuni
Itachengea dunia

141. Chukiipinga niushetwani
Undao kuvunda miyini
Ubagudhi kuusamini
A Mungu kuwakimbia

142. Dhindachuwenea lana
Huvadha kutukiana
Kupendana hakuna
Mwene kubarikia

143. Hufanyiana chuki
Biashara kudhishiriki
Kupacha ndruo hutaki
Udhalimu humfanyia

144. Wivu hufanyiana
Utukivu huvonyana
Mpaka kwa kurogana
Ushiriki kuubarikia

145. Ridhiki k'wa Mungu
Kumbuka nlimwengu
Hukuchiyae matungu
Ndruo kuitafudhia?

146. Haa chukianena
Haivi nkukosana
Usawa huvonyana
Upache kubakia

147. Haa kwambiana
Ndrio kupendana
Mana hurakibishana
Kama chwalivo usiwa

148. Haa huwabaini
Achutowe kidhani
Naalo usindidhini
Nae anyuke pia

149. Kupotea ndia
Ndrio kuyiva ndia
Basi kudhingatia
Naive muhimu

150. Kivumbe alobora
Ni aapukao ukora
Asikubali aujura
Aye kumvamia

151. Kivumbe atakao ubora
Ni asokapendi madhara
Kwa kudhishindra hasira
Kuto kukubali kumvamia

152. Kivumbe alo bora
Niaso katoi dharura
Yambo linalo nkera
Kero kulikimbia

153. Kalamu kwisha wino
Haamalidhiki maneno
Chuwandameni mifano
Avalo chuchangulia

154. Valichutolea ndia
Maina vakadhipachia
Ive rahisi kwechu chukia
Kuwavona avo mapicho

*Hiyo hiyo hee!*

## Shivulani ni Shaulani: Kiunji Cha Ine

1. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Mvumba dhivumbe
Akavapa akili

2. Vapache kuufahamu
Waubora wake Ilimu
Kwa bidii na hamu
Vatake kuitafudhia

3. Vayive umuhimu
Waavo majukumu
Na akuvaladhimu
Kuto akimbia

4. Vaukachae ujura
Vaukubali ubora
Nakila ladharura
Kulikumbachia

5. Vaitakie madhuri
Kwakudhivia jauri
Nakukachaa kiburi
Kuto kuvavamia

6. Vaipendelee udhima
Vaishi kwa usalama
Nakuva njema hatima
Itakapo kuvasikilia

7. Vadhamirie mema
Dunia vakiiyandama
Kwake Mola Karima
Vasiate kukaribia

8. Vakubali kuungana
Kuva ndrilo lamaana
Vakiripo kushikana
Umoya upache ndia

9. Ndriyo isi vaongwana
Mbiya chwalobikiana
Kwadhikao kuichana
Umoya kuudhingatia

10. Chwalipo sikia mbia
Mwicho chukauchikia
Kwechu upeche ndia
Umoya umechuyia

11. Lindaanda lisikome
Hata p'epo dhivume
Hakuna rahisi vaume
Bora ni njema nia

12. Kimbunga kuchusecha
Na kikukuu,dhitapicha
Kama ndrocho kuocha
Ukinyuka ikakimbia.

13. Bisumila chuifundre
Aubora chuchendre
Huu umoya uvandre
Ishina chukiubikia

14. Chuiyambie shari
Endra mbali yuviri
Wema undadhihiri
Bajunini kuchulia

15. Chuivilidhie heri
Kwa a Mola amuri
Atakuya madhuri
Kuchutapilia

16. Alombali naye karibu
Kufaulu eo chutulubu
Umoya ukiva wajibu
Baraka dhitachuyia

17. Ikiva nia ninjema
Achuyiva Rahima
Uvakao taudhima
Mocho wakidunia

18. Mwene nia mbovu
Akuchutakia maovu
Mola mwene nguvu
Basi humwangalia

19. Vataangamia vaovu
Venenao nia mbovu
Uvapache ivo uwovu
Venye kuchutakia

20. Chaloveko mwangoni
Kindashukiya maini
Nadhana dhimo ndani
Baharimi huowea

21. Kingodheecho nanga
Sichombo chantenga
Ch'atalibisi malenga
Mikondroni kuvukia

22. Ni chombo chakuvusa
Kisimaiyu na Mambasa
Darisalama kitaegesa
Dhechu kudhipakia

23. Chakuvusia Bajunini
Dhilidhoko uwaibuni
Na dhilidho makaoni
Ngome kudhijengea.

24. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Madhuri achupambe
Kwake hutegemea

25. Chwambe bisumila
Kwaisimu lake Mola
Kila lenyekuva naila
Rabi achuwepusie

26. Chumuombe Mungu
Mvumba malimwengu
Alilochubarikia fungu
Pache achuhifadhie

27. Achupambe chupambike
Miyini kwechu chukunduke
Nasi Vabajuni chufurahike
Baraka dhake dhikichuyia

28. Hutegemea kwake
Idhimwapo mivuke
Maudhiko aandroke
Mola akichusaidia

29. Chumuombe mweneedhi
Rabi Bwana Mungu nledhi
Kwechu akiveke kidhividhi
Ndio maovu asipache ndia

30. Nasi nachuichambuwe
Majukumu chuwatukuwe
Ubinafusi usichusumbuwe
Umoya wechu chukiubarikia

31. Chuubikie kiboma
Nchembo ulosimama
Ukuwe kwa salama
Hatari chukiukingia

32. Chuunosee nchembo
Chuivonee aurembo
Kinawiri lake pambo
Ruhu dhitachulia

33. Unyusie huu M'bajuni?
Ama hupuva usindidhini?
Ni dhichendro dhitabaini
Jawabu kuchupachia

34. Mana kigari chan'nadhi
Ni nkulima hukihifadhi
Vanama kina mbudhi
Vasipache kunvundia

35. Ndrio nchembo usiliwe
Pache kwaafiya ukuwe
Kwabidii mai unosewe
Uhai nguvu kuutakia.

36. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Mvumba dhivumbe
Kuichumia dunia

37. Chwambe bisumila
Kunchangulidha Mola
Chukinyuka chukiiyala
Kwake kutegemea

38. Chumuombe Haliki
Mvumba mahuluki
Kwake chutaradhaki
Mema kuchubarikia

39. N'dhuri wakuvumba
Misichu na nyamba
K'ungu na k'amba
Makao kuvavekea

40. Kachuecha duniani
Dhilidhoko aridhini
Nadhilioko baharini
Kuishi kuchusaidia

41. Wakuombwa ni Mungu
Mvumba ulimwengu
Kuishi valimwengu
Kachukadiria

42. Chuishi kwa imani
Upendo kuusamini
Chutaipacha amani
Nyoyo dhitachulia

43. Mema chuchendreni
Autukudhe Ubajuni
Barani na dhisiwani
Echu kuihifadhia

44. Lakutwa na lakuava
Dhikunduke mbava
Achaguke ote maliva
Akome kuchuvamia

45. Huhimidhwa chunyukeni
Chutokeni usindidhini
Chwamukie yambo gani?
Ni muhimu kudhingatia

46. Lengo na shabaha
Niiveko naswaha
Dhikiandroka karaha
Dhilidho chuvamia

47. Dhitaandrokae vavulana?
Ni wajibu kuvulidhana
Chwendre kwa kuyivana
Chuwandamapo ndia.

48. Bisumila sumi
Khele nadhivumi
Vadhee vangu imi
Valinirithisha

49. Uvuvudhi ni vuvuwao
Ni utungu imi nilo nao
Maovu chuchendrwao
Chukabakiwa na kulia

50. Hulia wala hachunyamai
Kama mwanguko wamai
Suluhisho hachulitumai
Chukakoma nasi kulia

51. Uvuvudhi mbwa kite
Kitokao ndrani matete
Imi pweke musiniate
Nisaidiani kuvuvuwa

52. Kuvuvuwa nisaidiani
Ghera nachufanyeni
Pamoya chuiyokoeni
Namacheso akidunia

53. Achukerao chuwadhivie
Pache maudhiko asie
Nsingi chuwavundie
Madhulumu alochuyia

54. Mmoya ave wavachu vote
Vote mmoya vasimuwate
Mana ndrue mbeu ni nte
Dhitoseepo nkumoya

55. Dhitosee nchini
Makao ni aridhini
Midhi iko ntangani
Ishina kulinosea

56. Shikani shivu chukinena
Chuvuvuweni vaongwana
Vachusikie vechu vana
Vaiyandame echu ndia

57. Mwiva huva ntunga
Kheva kamea munga
Litavona ito likienga
Livalo kushuhudia

58. Jukumu chutukueni
Huu umoya kuubuni
Mabadiliko Bajunini
Achengedhe ndia.

59. Bisumila chwambe
Dhibikwapo pembe
Nliyo na uchambe
Valombali kuusikia

60. Chwambe mema
Alochuvonya mama
Achupende Karima
Hishima kunvekea

61. Alochufundra baba
Chwambe sihaba
Achupende Rabba
Hishima kunvekea

62. Chwambe matamu
Avadhee vakarimu
Achupende Halimu
Hushima kuvavekea

63. Kisha chwambe echu
Andrimini mwechu
Kuuchambuwa uchu
Shime kubarikia

64. Na vana vakiamba
Chusivavelee simba
Kuvasikia naomba
Dorini kuvavuchia

65. Alochwambia Wadudi
Na anchume Muhamadi
Ni ladhima huchubidi
Kwandama nakubarikia

66. Hidhi dhikiva ngudho
Dhitachupa uwedho
Wakuva na mavadho
Akili kudhikombowa

67. Uwongodhi wa Kibajuni
Eo chuupeeo sukani
Vabajuni chuusaidieni
Safari kuusahilishia

68. Namba chusisahauni
Aubajuni madhumuni
Chusitokeni ndiani
Mashakani chutaumia

69. Chundaanda chusikome
Chukadhe kamba vaume
Atapiyapo nachi t’ume
Mena kumwongojea

70. Amakosa akifanyika
Siumoya kuvundika
Niudhaifu hudhihirika
Ichuladhimu kuudhivia

71. Madhuri akifanyika
Niuchu chwautaka
Ubinadamu hubainika
Palee chukiubarikia

72. Usawa ukichendreka
Haki itachambulika
Udhalimu utachuepuka
Alomadhuri kuchuyia

73. Madhuri chukiakubali
Utachwandrokea ujahili
Dhidhivilike ndia batili
Na chuki dhitakimbia

74. Dhikikimbia chuki
Dhitaandroka dhiki
Upache ndia urafiki
Upendo kuubarikia

75. Makao chwalo abuni
Kwechu isi Vabajuni
Usalama na amani
Ndrio huwatakia

*Hiyo hiyo hee!*

## Shivulani ni Shaulani: Kiunji cha Tanu

1. Bisumila chwambe
Vasikie dhivumbe
Shango na Vumbe
Vadhee valichwatia

2. Valichwatia chulime
Napia siki chugeme
Pache ndaa ikome
Milangoni kutapia

3. Valichwatia chuvinde
Na vanama chutinde
Amuri chusivunde
Madhambi kuitakia

4. Chakula chule chechu
Chusintegemee nchu
Ndaa isitapie kwechu
Kuya kuchuvamia

5. Chaafia ndriyo chule
Kama vadhee vakale
Chasumu katu chusile
Kuidhuru echu afia

6. Magonjwa achuiyeo
Kila aina achupachao
N’nyani haa ayivao
Ndia gani amechuyia?

7. Haa chuwadhingatieni
Na chuwachieni akilini
Kudhimbiria tamaduni
Utwevu chumeitakia

8. Kutoyiva ulacho
Chalivukae ncho
Afiani ni mocho
Kuramba huitakia

9. Ulapo usicho kakiyisi
Hukuvelea tamu uyusi
Usiyive kuva ni najisi
Uchafu kaubugia

10. Ulapo usicho kakiyisi
Chalilimwae usidadisi
Basi ndaivelea p’isi
Uyusi huubugia

11. Asokavoni ntongo
Aishio bila malengo
Auvonao nlango
Huvonywi ndia.

12. Bisumila chwambe
Uwovu wach’embe
Kudhuru dhivumbe
Huwatiwae ndia?

13. Dhiyieye chuvulidhe
Valindi vachweledhe
Vachujibu vasipudhe
Hukosae kudhidhivia?

14. Huwangamidha dhidhadhi
Kwa kuwatwa vachurudhi
Kudhidhanya wadhiwadhi
Vasipache wakuvadhia

15. Chwambieni chuyive
Huwatwae kwechu live
Valindi valivoko vasive
Miyini vatalidhivia?

16. Nasi nihatuwa gani
Chutukudhie Vabajuni
Kuuwondrowa uhuni
Huu ulo chuvamia?

17. Hufanywa kwechu miyini
Na nivana vechu vahuni
Ni hatuwa gani Vabajuni
Ambao isi huidhingatia?

18. Vangine chukivalaumu
Nasi ive chutafahamu
Nilipi lechu isi jukumu
Hili yambo kulidhivia?

19. Chunyemee hachuachayi
Huchuvundia echu miyi
Huutedha vaubikao ntoyi
Kwa mato chukivaangalia

20. Sitaufunga ulimi
Na kutiriri sikomi
Haa hunidhuru imi
Vana vakiangamia

21. Hili yambo siichocho
Kwakweli lina udhicho
Miyini lichidhie mocho
Dhidhadhi huwangamia

22. Mila ndaiharibu
Liesee dharubu
Ndaenedha aibu
Dini huchuchafulia

23. Hii ninjama anyani
Kuukudha huu uhuni
Jawabu chulitakeni
Achwambie ayivao

24. Sirikali chuivulidheni
Jukumu hili ndanyani
Hungiyae hapa nchini
Isiwedhe kudhidhivia?

25. Chwambe alositamana
Apache sasa kuyivikana
Vaafanyao vangasitana
Vayivikana navambia

26. Navaumbuliwe vaumbuke
Siri dhavo dhidhihirike
Sirikali ifanye kadhi ake
Mihadarati kuidhivia

27. Hii nibiashara ambani
Hata vave havavonekani?
Musinyamae chwambieni
Atani kuchunyamalia

28. Chumechoka kuvasikia
Muchwambiyao audhia
Hii mihadarati kuidhivia
Indashindrwa Sirikali?

29. Basi uhuru chupeni
Na p'eo chukidhini
Mwandroke ndiani
Chupache kuipea

30. Chuupee uchafu
Uwondroke udufu
Na kila muharibifu
Chunvonye ndia

31. Avone ndia aandroke
Kwa amani ikubalike
Kwa nguvu asitake
Miyi kuchuchafulia

32. Chusinyamaeni tena
Kimwa hukudha lana
Ukweli chukiunena
Upache vakuusikia

33. Kimwa vaongwana
Chikidhidi ayivikana
Kina maneno hunena
Vakae valichwambia

34. Nimaneno gani nambiani
Pache nami nitoke kidhani
Mmema ao maovu vendani
N'nyani tanidokedhea?.

35. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Haombwi kivumbe
Ene kuwakadiria

36. Amola chuwashitahi
Chuntukudhe Ilahi
Ayao ene makuruhi
Chuwadhivieni ndia

37. Kwa lake Mola isimu
Chuombeni matamu
Dhidhivilike sumu
Kwechu kuchuyia

38. Utamu wabusara
Makosa ave hasara
Usawa uve nibora
Haa kudhingatia

39. Utamu wafikira
Chuupinge ukora
Chudhijali dharura
Haa kuwabarikia

40. Sumu ni mavadho
Akukudha mivodho
Kumbiriwa kiedho
Ukavekwa mpini

41. Kiedho bila ampini
Kadhi taichendrani?
Mpini unafaida gani
Kiedho ukikimbiria?

42. Sumu dha akili
Nimaovu maadili
Uchafu kuukubali
Miyi kuchuvundia

43. Maumbile a Mola
Haambiwi lahaula
Mwene kuchia ila
Upotedhee ndia

44. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Asiomoke maombe
Isi kuchwangukia

45. Akichomokea maombe
Chutaumia dhivumbe
Kwake Mola chuombe
Madhara kuchwepusia

46. Chumuombe Manani
Achuhifadhi maishani
Nachukendra kaburini
Nuru ake kuchuvalia

47. Tamaduni chuhifadhini
Dhote dhenye samani
Vana chuvafundrisheni
Dhisipache kupotea

48. Kuchema na kulima
Kuvinda na kutoma
Kuundra na kugema
Uyudhi wechu ubakie

49. Uyachi chusiusahauni
Dhibiriti dhamadukani
Ndrio chukadhisamini
Uwinga ukachuvamia

50. Uvumbudhi wakibajuni
Chusiukoseshe samani
Chusokaayisi vendani
Uchumwani akachuchia

51. Ntawala hatawaliwi
Ela asokaichambuwi
Aifahamuo haambiwi
wake kuushikilia

52. Maganga na akili
Ni ushauri kamili
Valinena vaasili
Isi chudhingatie

*Hiyo hiyo hee!*

## Shivulani ni Shaulani: Kiunji cha Sita

1. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Mvumba dhivumbe
Na it'idhe sabaa

2. Mvumba suni nadhiombe
Mbudhi,kuku na ng'ombe
Mawiwi,yiri na dhidhimbe
Kuitembea hii dunia

3. Kachuvumba dhivumbe
Kachwechea na ujumbe
Kuundra soli na yembe
Uyudhi kachupachia

4. Iti anane hwamba
Nichujengao majumba
Na miyi kuipamba
Vadhee havakukosea

5. Ichaywao it'i anane
Nihondre na mangine
Ni kufuru asinene
Asiye kudhingatia

6. Kuva alichuvumba
Chuchendrao namba
Niuwedho wamuumba
Ufahamu kuchupachia

7. Ndrio it'i anane
Ndechu chusinene
Ambae udengene
Asiche kuvulidhia

8. Kama niuwedho wako
Mbona milele usiveko
Uwatadho dhisive dhako
Vangine vakaichwalia?

9. M'bajuni ninchu mwelewa
A Mungu huwachambuwa
Kadari isi chwaliandikiwa
Chuiyandame chukisikilia

10. Chukisikilia duniani
Kadari chuiyandameni
Kuruwani ndrio sukani
Tamaduni chukibarikia

11. Kujenga miyi na kubuni
Aridhini napia baharini
Achendrao M'bajuni
Mungu alimpangia

12. Ndrivo chuwaminivo
A Mungu chuelewavo
Vafasiri vatafusirivo
Kufuruni hachutangia

13. Huku chuwaminivo kwechu
Chubuniyo hachuneni ndechu
Mana chwalivumbwa vachu
Kuya Mola kunchumikia

14. Nsomi kiva hafahamu
Na halielewi hili ilimu
Nashike tena kalamu
Arudi kulidhingatia

15. Tafusiri ni ningi
Dhaik'akwa na ingi
Ntunga hauvi ntungi
Mai chungauchilia.

16. Bisumila chwambe
Pwekee chumuombe
Aeneeo kila p'embe
Ilahi Mola Jalia

17. Chumuombe alo mema
Aridhiki na ausalama
Matonyi na mak'ulima
Apache kuchubarikia

18. Mvumba mbeu na michi
Mayungu na machikichi
Na ilimu lamocho uyachi
Ndrie wakuntegemea

19. Na mahitaji echu
Haatoki kwa nchu
Alovumba vachu
Ndrie huwajaalia

20. Ni uwedho wa Rabana
Chufanyao kuwedhekana
Verevu chungaivona
Huchuhadaa dunia

21. Vaipao VAVE makosa
Kwailimu lavo lakisasa
Isi havatachuwasa
Hishima kuivekea

22. Vadhee kuvahishimu
Kimila huchuladhimu
Kwa dini nijukumu
Nasi hubarikia

23. VAVE ni nyimbo
Habari ene pambo
Mapicho aurembo
Aubajuni kubakia

24. Wa VAVE mpango
Ukidhiyiva dhilingo
Utauvona nlango
Mapicho kuwapichia

25. Nimaneno matamu
Aakili dhilidho timu
Maana kuwafahamu
Kwa mwalimu vulidhia

26. Wake ufahamu
Ni ilimu muhimu
Kuyiva huladhimu
Lilipo kulandamia

27. VAVE nik'umbusho
Ilomeya k'orosho
Ibiboni siyo mwisho
M'bibo huchuhifadhia

28. M'bibo kudhawa
Tandu ukatukuwa
Nakuva kidhao iyuwa
Midhi ilichangulia

29. Echu VAVE nikitabu
Kilo sahihika irabu
Kuyiva wakutulubu
Niilimu kwandamia

30. Nimaneno adhahabu
Aakili dhilidho tubu
Maana siaharibu
Kuyiva vulidhia

31. Wa VAVE udhuri
Hauchambui biri
Kuukubali nihiyari
Aladhima nda Jalia

31. VAVE ni nguvo
Avapendao avo
Kuwasitiri alivo
Alo changulia

32. Nisitara aubajuni
Mbeu autamaduni
Ake VAVE samani
Isi huikumbachia

33. VAVE ndricho kiyoo
Muenge ndrie hoo
Sisarakasi sishoo
Nihakika huvambia

34. VAVE chuyive nisati
Dhavalo itembea iti
Dhilidhopicha nyakati
Ufahamu kuchwatia

35. VAVE ndrio sura
Atamaduni bora
Hifadhi nibusara
Ipache kubakia

36. VAVE nayiva niulimi
Wavadhee vangu imi
Kina Mahadhi ami
Valo changulia

37. Nasi na chuhifadhini
Dhavadhee tamaduni
Utukuke huu Ubajuni
Hapa kwene dunia

38. VAVE ndrio sauti
Avalo dhishika iti
Valopicha Vanati
Nasi kuvasikia

39. VAVE ni maneno
Aliyo dhaa mifano
Ukulima na mavuno
Ilimu kuchuwatia

40. Kuhifadhi live jukumu
Kwechu isi dhavo damu
Lisichupotee hili ilimu
Lavalo chuchangulia

41. Kuishika nachutake
Pache isichushopoke
Libakie ilimu lake
Kuchuvonya ndia

42. Kuipenda chubarikie
Uhifadhi chuitakie
Vatavokuya vaisikie
Ivavonye navo ndia

43. Kuhifadhi chuladhimike
Pache VAVE udhuri wake
Ulimwenguni uchambulike
Hishima kuchuvekea

44. Yoo VAVE yoo
Nichudha kiliyo
Hukulilia moyo
Matodhi haakubakia

45. Sikilo cha hudhuni
Nifuraha ilo nd rani
Kuva nsingi, Ubajuni
Kuchuhifadhia

*Hiyo hiyo hee!*